**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

Kumb Na. TCC/CT/A55/3 Tarehe: 03 /01/2024

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Mkurugenzi wa Jiji la Tanga anapenda kuwatangazia nafasi za kazi **(386)** za muda za ajira ya mkataba kwa watanzania wenye sifa waweze kuomba. Nafasi hizo ni kama ifuatavyo:-

## 1. MKUSANYA USHURU NA MAPATO NAFASI (79)

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Muombaji anapaswa kuwa na cheti cha kidato cha nne/sita
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (smart phones)
- Waombaji wenye mafunzo ya Jeshi la akiba watapewa kipaumbele.

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kukusanya ushuru katika eneo utakaopangiwa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Tanga
- Kutunza kumbukumbu za hesabu
- Kutunza vizuri mashine za kukusanyia mapato (POS)
- Kuwasilisha makusanyo katika akaunti za Halmashauri
- Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Halmashauri.
- Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na msimamizi wako wa kazi.

## 2. KITENGO CHA BUSTANI NAFASI SITINI NA MBILI (62)

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Muombaji ajue kusoma na kuandika.
- Awe na kitambulisho cha NIDA

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kuzalisha/kuotesha maua kwenye kitalu cha Jiji
- Kupanda maua, na miti ya kivuli kwenye maeneo ya Bustani za Jiji
- Kupalilia maua, kulimia visahani, kutengeneza mishazali na kulimia maeneo ya wazi
- Kukata maua, kukata na kupunguzia matawi miti ya maua
- Kufyeka ukoka kwenye maeneo ya Bustani na kufyeka nyasi kwenye maeneo ya wazi.
- Kumwagilia maua yote yaliyopandwa.
- Kuweka mbolea kwenye maua yote yaliyopandwa.

**3. KITENGO CHA MIFUGO NAFASI (03)**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (smart phones)

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Usafi wa eneo la machinjio ndani na nje ya maeneo yote yanayozunguka eneo la machinjio (kila siku).
- Kufyeka mazingira yote yanayozunguka machinjio.

**KITENGO CHA UVUVI NAFASI (07)**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji awe anajua kusoma na kuandika.
- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Maombi yaambatanishwe na kimojawapo ya kivuli cha cheti kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA na picha moja ya passport Size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote



CamScanner

- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (smart phones)

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kukusanya takwimu za mauzo ya Samaki.
- Kufanya doria/ukaguzi wa vibali.
- Kusimamia utoroshaji wa mazao ya uvuvi.
- Kufanya doria za uvuvi haramu kwa kushirikiana na afisa uvuvi

## 4. UDHIBITI WA TAKA NAFASI (118)

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji awe anajua kusoma na kuandika.
- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Ufagizi wa barabara na maeneo mengine
- Kutunza vituo vya taka( skip backet)
- Kusafisha mifereji ya maji na mvua
- Kuzoa taka kwa kutumia magari

## 5. KITENGO CHA BUSTANI NAFASI (62)

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji awe anajua kusoma na kuandika.
- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size..
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kuzalisha/kuotesha maua kwenye kitalu cha maua cha Jiji
- Kupanda maua, ukoka na miti ya kivuli kwenye maeneo ya bustani za Jiji
- Kupalilia maua, kulimia visahani, kutengeneza mishazali na kulimia maeneo ya wazi
- Kukata maua, kukata na kupunguza matawi ya miti na kufyeka nyasi kwenye maneo ya wazi



CamScanner

- Kumwagilia maua yote yaliyopandwa
- Kuweka mbolea kwenye maua yote yaliyopandwa

6. IDARA YA UJENZI NAFASI (22)
    - Wasanifu majengo nafasi – 7
    - Operator wa mitambo nafasi 6
    - Karakana nafasi – 4
    - Umeme nafasi – 4
    - Mpima mizani nafasi – 1

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Muombaji anapaswa kuwa na cheti cha kidato cha nne/sita
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote
- Awe amesoma chuo chochote cha ufundi wa magari, Umeme, Majengo n.k

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kukarabati mifumo ya maji kwenye majengo ya Halmashauri
- Kusaidia shughuli mbalimbali za ujenzi kwenye miradi ya Halmashauri panapohitajika
- Kufanya kazi za barabara, viwanja vya shule na wengine wanaendesha magari ya idara mbalimbali kwa majukumu ya Halmashauri ya Jiji
- Kutengeneza magari/mitambo yote ya Halmashauri ya Jiji pamoja na ku servise jenerator na mashine za tofalui block machine na kazi nyingine zinazojitokeza karakana
- Kurekebisha hitilafu za umeme majengo yote ya Halmashauri ya Jiji
- Kusuka mifumo ya umeme pale inapohitajika
- Kukarabati miuondombinu ya taa za barabarani na taa za kuongoza magari
- Kukusanya ushuru wa mizani depot

**7. KITENGO CHA UHIFADHI MALIASILI NA MAZINGIRA NAFASI 22**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania.
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho:- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size.
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote



CamScanner

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kuandaa eneo kwa ajili ya upandaji miti katika msimu husika
- Kupanda miti (mitiki)
- Kufanya usafi wa shamba
- Kupunguza matawi (pruning)
- Kuokota mbegu
- Kulinda na kutunza shamba la miti

**8 SEKTA YA ARDHI NAFASI**

- Wapima wasaidizi - 6
- Warasimu ramani - 2
- Wahudumu - 2
- Wathamini wasaidizi - 1

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Muombaji anapaswa kuwa raia wa Tanzania
- Umri wa muombaji kuanzia miaka 18-45
- Muombaji anapaswa kuwa na cheti cha kidato cha nne/sita
- Maombi yaambatanishwe na kivuli kimojawapo kati ya kifuatacho.- cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha mpiga kura na picha moja ya passport size
- Muadilifu asiye na kasoro yeyote
- Awe amesoma chuo chochote cha masuala ya Ardhi na Uthamini

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kusaidia utambuzi wa mipaka ya viwanja vilivyopimwa chini ya msimamizi wa mpima ardhi.
- Kusaidia kuonyesha kwa wateja viwanja vipya vilivyopimwa na kuuzwa katika miradi ya Halmashauri.
- Kuwasaidia wapima ardhi katika utekelezaji wa mazoezi ya upimaji yanayoratibiwa na Halmashauri ya Jiji.
- Kusaidia kuandaa michoro ya hati (Dee plan)
- Kusaidia kuandaa ramani za upimaji (Survey plan)
- Kufanya ukaguzi wa hali ya uwandani (site) na kuwasilisha ramani.
- Kusaidia kuonyesha mipaka kwa ajili ya kurudisha ramani.
- Kufanya uthamini na kuandaa taarifa za uthamini
- Kufanya makadirio ya kodi/uhamisho wa umilikishaji na umilikishaji upya.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono, zikiwa na anuani kamili ya mwombaji, namba ya simu na zipitie kwa Mtendaji wa Kata anayoishi.



CamScanner

Maombi yote yawasilishwe kwa -

Mkurugenzi wa Jiji,
09 Barabara ya Hassan Ngw'ilizi,
21101 Central Tanga,
S L P 178,
**TANGA**

***Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/01/2024 saa 9.30 mchana.***

Saidi M. Majaliwa
**MKURUGENZI WA JIJI**

MKURUGENZI WA JIJI TANGA